# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu. 03-3425-4531 FAX. 03-3425-7844
Barua pepe: tzrepjp@tanzaniaembassy.or.jp
tokyo@nje.go.tz

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
21-9, KAMIYOGA 4-CHOME.
SETAGAYA-KU, TOKYO 158-0098

# TAARIFA

## FURSA MBALIMBALI ZA UFADHILI WA MASOMO NA TAFITI ZILIZOPO NCHINI JAPAN *(SCHOLARSHIPS FOR INTERNATIONAL STUDENTS IN JAPAN)*

Ubalozi unapenda kutoa taarifa kuhusu uwepo wa fursa mbalimbali za ufadhili wa masomo na tafiti nchini Japan, zinazotolewa na Serikali ya Japan na wadau wengine wa maendeleo waliopo Japan, kama ifuatavyo:

i) **Serikali ya Japan** kupitia *Wizara ya Elimu, Utamaduni, Michezo, Sayansi na Teknolojia (MEXT Scholarship)*;

ii) **Programu za Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA)** – programu za JICA hutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa umma, wataalamu, wanasayansi na viongozi wa taasisi mbalimbali kutoka Tanzania;

iii) **Mashirika binafsi ya Kijapani** yanayotoa ufadhili wa kujitegemea kwa wanafunzi wa kimataifa; na

iv) **Vyuo vikuu** vinavyotoa ufadhili moja kwa moja *(*University-Specific Scholarships) kwa wanafunzi wa kimataifa.

Sehemu kubwa ya ufadhili huu unalenga masomo kwa ngazi ya Umahiri *(Master's)* na Uzamivu *(PhD).* Aidha, Wizara ya Elimu ya Japan hutoa ufadhili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza *(Undergraduate)* na Masomo ya Ufundi *(Specialized Training)**.***

Kwa taarifa zaidi kuhusu fursa hizo zikiwemo, sifa za waombaji na taratibu za maombi, tafadhali tembelea tovuti:

a) UBALOZI WA TANZANIA NCHINI JAPAN: https://www.jp.tzembassy.go.tz/resources/view/taarifa-ya-fursa-mbalimbali-za-ufadhili-wa-masomo-na-tafiti-zilizopo-nchini-japan-scholarships-for-international-students-in-japan

b) UBALOZI WA JAPAN NCHINI TANZANIA: https://www.tz.emb-japan.go.jp/itprtop_en/index.html

c) *STUDY IN JAPAN – Scholarship Pamphlet*: https://www.studyinjapan.go.jp/en/planning/brochures/#002

Tunashauri Watanzania wenye nia ya kusoma au kufanya tafiti nchini Japan **kutembelea tovuti hizi mara kwa mara** ili kubaini fursa mpya zinapowekwa kwa mwaka husika wa masomo. Ubalozi unatoa rai kwa Watanzania kuchangamkia fursa hizo, zinapotangazwa.

**UBALOZI WA TANZANIA NCHINI JAPAN**
**TOKYO**
**11 NOVEMBA 2025**